**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA**

NENO LA UFUNGUZI KUTOKA KWA KAMISHNA WA BIMA KATIKA MAFUNZO KUHUSU UKIMWI NA RUSHWA

TAREHE 01 FEBRUARI 2024

UKUMBI WA TAGLA, DAR ES SALAAM

**Ndugu,**
**Menejimenti ya Mamlaka**
**Watumishi wote**
**Watoa mada**
**Wageni Waalikwa**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

***KWANZA*** kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai aliyotujalia na kuweza kukutana tena hapa leo!

***PILI*** nipende kuwapongeza watumishi wote mlioamua kuhudhuria katika mafunzo haya siku ya leo, mmefanya uamuzi sahihi kwasababu wakati wote unapopata fursa ya kupata elimu ni vizuri kuitumia, sababu elimu ni maarifa na ujuzi.

**Pia elimu hii** mtakayoipata leo itawakumbusha kuhusu kulinda afya zenu hasa kwa magonjwa ambayo mnaweza kujikinga nayo kama HIV, kwa ustawi wenu wenyewe na taifa letu.

Ikumbukwe afya njema ni msingi wa maisha yetu kwasababu;

- **Inaongeza ufanisi wa maisha:** Afya njema inakuwezesha kufanya kazi zako za kila siku kwa ufanisi zaidi. Bila afya nzuri, inaweza kuwa vigumu kutekeleza majukumu yako ya kila siku au kufurahia maisha.
- **Kuzuia Magonjwa**: Wakati una afya nzuri, mwili wako unakuwa na uwezo wa kupambana na magonjwa mbalimbali na kuwa na kinga imara.
- **Inaongeza ushiriki wa shughuli mbalimbali katika jamii**: Afya njema inakusaidia kufurahia maisha yako kikamilifu. Unaweza kushiriki katika shughuli za kijamii, michezo, na matukio bila kuathiriwa na maumivu au matatizo ya kiafya.

- **Kupunguza Mzigo wa Gharama za Matibabu**: Wakati unapokuwa na afya njema, unajikinga na gharama kubwa za matibabu
- **Ustawi wa afya ya akili**: Mtakubaliana na mimi kwamba magonjwa yanaleta msongo wa mawazo ‘stress’ kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kimwili na kijamii

Kwa hiyo, afya njema siyo tu inahusiana na mwili wako, bali pia inagusa upande wa akili, hisia na maisha yako kwa ujumla.

Lakini pia mtapewa somo kuhusu rushwa na namna ya kujikinga nayo, wakati wote ni muhimu kukumbuka misingi ya Utumishi wa Umma kwa kufuata sharia, kanuni na taratibu zilizowekwa.Ikiwemo kutokutoa wala kupokea rushwa, kwasababu rushwa ni adui wa haki na adui wa ustawi katika utumishi wako.

**TATU** niwapongeze sana waandaji wa Mafunzo haya ambayo yanagusa maeneo muhimu ya maisha yetu ambayo ni afya na uadilifu.

Kwasababu kuna kazi na maisha mengine na ni lazima wakati wote mzani uwe sawa yani kuwe na ***“Work, life balance”***

Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Nawapongeza sana kwa hili.

## 1. NINI UMUHIMU WA MAFUNZO HAYA YA UKIMWI NA RUSHWA

### 1.1 Kwa upande wa Afya

Mafunzo haya yana umuhimu mkubwa kwa kwa ustawi wa taasisi na mtu mmoja mmoja, kuwa na mtumishi mwenye afya njema ni kuwa na ufanisi mzuri pia katika kazi zetu ili kufikia malengo tuliyojiwekea na ya Serikali yetu kwa ujumla.

Lakini pia familia zetu zinatutegemea ni muhimu kukumbuka hilo kila wakati na kuepuka magonjwa ambayo yanasababishwa na mitindo mbalimbali ya maisha yetu ya kila siku ***“lifestyle”*** wewe kama baba, mama au mtoto kwa mzazi wako ni jukumu lako kuilinda afya yako ili kuweka misingi imara na kutekeleza majukumu katika nafasi husika.

Aidha mafunzo haya yatatusaidia au kutukumbusha namna ya kujikinga na magonjwa haya na wataalamu wetu watatupa takwimu mbalimbali za hali ya UKIMWI nchini na kujua kama taifa tupo wapi lakini muhimu zaidi ni kujua kitu gani cha kufanya kujikinga na kuwa na afya bora.

**1.2 Kwa Upande wa Rushwa**

Wengi wenu mliopo hapa ni vijana, zipo tamaa nyingi katika maisha ambazo mnapaswa mshindane nazo na kuridhika na mlivyo navyo huku mkitafuta ziada kwa njia halali bila kuumiza maisha ya mwingine

Katika kazi zenu za kila siku katika sekta yetu ya bima ni ukweli usiopingika mnakutana na vishawishi vya kupokea rushwa, lakini niwakumbushe Serikali imewaamini na kuwapa nafasi hizo ili mfanye sahihi. Lakini pia ‘mkono wa serikali ni mrefu’ na Serikali ya Awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imejizatiti kupambana na vitendo vya rushwa.

Hivyo na sisi tuiishi kauli yetu ya “**TIRA KWA SOKO SALAMA LA BIMA”** tukikataa kwa nguvu vitendo vya ulaghai na rushwa.

**NI RAI YANGU**, msikilize kwa makini mafunzo haya, kila mmoja atoke hapa akiwa amebeba maarifa na kuyatumia kwa faida yake mwenyewe, wanaomtegemea na taasisi yetu kwa ujumla.

Asanteni sana kwa kunisikiliza!

**BAADA YA KUSEMA HAYO NITAMKE: MAFUNZO HAYA YAHUSUYO UKIMWI NA RUSHWA YAMEFUNGULIWA RASMI.**